# Dhima za Mbinu Linganishi katika Kuhusisha Lugha na Lahaja

Pendo Mwashota

**Ikisiri**

Lengo la makala hii ni kujadili dhima za Mbinu Linganishi katika kuhusisha lugha na lahaja. Data za makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu mbalimbali ambazo ni usaili, ushuhudiaji, hojaji na majadiliano katika majopo. Utafiti ulifanyika Tanzania Bara hususan Mkoani Mtwara na Tanzania Visiwani katika maeneo ya Pemba na Unguja. Utafiti umeongozwa na Nadharia ya Isimu Historia-Linganishi iliyoasisiwa na William Jones (1786). Katika makala hii nadharia hii imetumika kwa sababu suala linalozungumziwa linahusu Mbinu Linganishi hususan dhima zake katika kuhusisha lugha na lahaja. Matokeo ya utafiti wa makala hii yamebaini kuwa Mbinu Linganishi ina dhima mbalimbali katika suala zima la uhusiano baina ya lugha na lugha, na lugha na lahaja. Mbali na dhima hizo makala imebaini kuwa mbinu hiyo ina mipaka mbalimbali ambayo haina budi kuzingatiwa wakati wa kuhusianisha lugha au lahaja. Hii inatokana na kwamba wanaisimu wengi wamejikita katika kulinganisha lugha za Kibantu na Kiswahili huku wakisahau lahaja za lugha za Kibantu ambazo baadhi ya wanaisimu kama vile MLUTA (2009) wameziainisha kama lugha kamili ilhali baadhi ya wanaisimu kama vile Kraal (2005) na Amani (2010) wanazichukulia kama lahaja[1]. Makala hii imeweka bayana kuwa ni vema ulinganishi wa lugha za Kibantu na lahaja zake ukachukuliwa kwa umakini mkubwa kwa sababu haitoshi kutoa mahitimisho yasiyo na uthibitisho kuwa lugha fulani zipo katika kundi moja ilhali zinatofautiana. Pia, imependekezwa kuwa ipo haja ya kufanya uchunguzi wa kina wa lugha za Kibantu na lahaja zake kwa kutumia Mbinu Linganishi ili kuibuka na matokeo toshelevu yatakayotuwezesha kuainisha vema lugha za Kibantu na lahaja zake[2].

## 1.0 Utangulizi

Lengo la makala hii ni kujadili dhima za Mbinu Linganishi kama nyenzo inayotumiwa na wanazuoni mbalimbali wa lugha za Ulaya, Afrika na kwingineko katika kubainisha uhusiano baina ya lugha. Data za makala hii zimekusanywa mwaka 2016 nchini Tanzania. Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data ni usaili, hojaji, ushuhudiaji na majadiliano katika majopo. Utafiti ulifanyikia Tanzania Bara (mkoani Mtwara) na Tanzania Visiwani (Pemba na Unguja). Maeneo ya mkoa wa Mtwara yaliyohusika ni wilaya ya Mtwara Vijijini na Manispaa ya Mikindani. Kwa upande wa Tanzania Visiwani data zilikusanywa katika Kisiwa cha Pemba mathalani katika wilaya ya Mkoani, Wete na Micheweni, na Unguja katika mkoa wa Unguja Kusini katika maeneo ya Makunduchi, Paje, Kae Kuu, Mtende, Tasani na Jambiani. Kwa upande wa Mtwara, mtafiti alikusanya data za lugha ya Kimakonde, kwa upande wa Pemba alikusanya data za lugha ya Kipemba, na kwa upande wa Kusini Unguja alikusanya data za lugha ya Kimakunduchi.

---

[1] Mfano mzuri ni Kimalaba (lahaja mojawapo ya lugha ya Kimakonde). Kwa ufafanuzi zaidi tazama Kraal (2005) na Amani (2010).

[2] Hapa ina maana ya lahaja zilizopo katika lugha mbalimbali za Kibantu tofauti na Kiswahili. Lahaja zinazozungumziwa hapa ni tofauti na lahaja za Kiswahili.

Utafiti umeongozwa na Nadharia ya Isimu Historia-Linganishi iliyoasisiwa na William Jones (1786). Jones alianzisha nadharia hiyo katika mhadhara wake uliohusu lugha ya Kisanskriti. Alibaini kuwa Kiyunani, Kilatini na Kisanskriti zinaelekea kuwa na chimbuko moja. Mbali na mambo mengine lugha hizo zilionekana kuhusiana na Kipashia, Kigothiki na Kiseltiki. Aidha, Luraghi na Bubeniki (2010) wanaeleza kuwa matini za Jones hazioneshi wazi kwamba lugha hizo ni za Mame lugha-moja. Tafiti zilizofuata baada ya Jones za baadhi ya wanaisimu kama vile Bopp (1816), Grimm (1822), Schleicher (1850, 1861 & 1873), Verner (1875) na nyinginezo ndizo zinazoonesha kuwa baadhi ya lugha zilizotajwa na Jones ni za Mame lugha-moja. Ni kutokana na tafiti za wataalamu hao ndipo kukaibuliwa Mbinu Linganishi iliyotumika kuhusianisha lugha na lahaja mbalimbali ili kubaini kama zinatokana na chimbuko moja au la. Katika makala hii nadharia hii imetumika kwa sababu suala linalozungumziwa linahusu Mbinu Linganishi, mathalani dhima zake katika kuhusisha lugha na lahaja. Makala hii imegawanyika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambao unaelezea lengo la makala, eneo na mbinu za utafiti, nadharia iliyotumika na fasili ya lugha na lahaja. Sehemu nyingine zilizobaki zinahusu fasili na chanzo cha Mbinu Linganishi, dhima za Mbinu Linganishi, mipaka ya Mbinu Linganishi na hitimisho.

Ni vema tufasili dhana ya lugha na lahaja kwa sababu zinahusiana na makala hii. Wataalamu mbalimbali wamefasili dhana hizi. Katika makala hii tutadondoa fasili za baadhi yao kama vile Mekacha (2011), Hans (2014) na Massamba (2016). Mathalani, Mekacha (2011: 3) anaeleza maana ya lugha kuwa ni nyenzo ya mawasiliano, yaani chombo kinachowawezesha watu wa jamii moja na wa jamii tofauti kuwasiliana, kupeana taarifa na kuelewana. Anafafanua zaidi kwa kusema kuwa lugha ni kiungo (i) kati ya mtu na mtu, (ii) kati ya mtu na jamii, (iii) kati ya jamii au taifa na jamii au taifa jingine, na (iv) kati ya mtu/jamii na mazingira yake halisi na ya kufikirika. Naye Massamba (2016: 64) anafasili kuwa lugha ni mfumo wa sauti nasibu ambazo zimebuniwa na jamii kwa madhumuni ya mawasiliano kati yao.

Kuhusu lahaja, Massamba (2016) anaeleza kwamba ni lugha mojawapo kati ya lugha ambazo kimsingi huhesabiwa kuwa lugha moja isipokuwa zinatofautiana katika mambo madogo kama lafudhi au msamiati usiokuwa wa msingi. Kwa upande wake, Hans (2014: 14) anafasili lahaja kuwa ni kilugha kinachojipambanua katika msamiati (usiokuwa wa msingi), matamshi, maumbo na maana za maneno pamoja na kanuni za miundo miongoni mwa wazungumzaji wa lugha zenye asili moja. Hans anaendelea kufafanua kuwa tofauti katika msamiati huo (usiokuwa wa msingi) inaweza kujibainisha zaidi katika ngazi ya fonolojia (ambapo maneno yanaweza kutofautiana katika baadhi ya sauti lakini yakiwa na maana moja) au katika ngazi ya semantiki (ambapo maneno tofauti yanaweza kutumiwa kueleza dhana moja au dhana mbalimbali kuelezwa kwa neno moja).

Katika makala hii, lahaja inafasiliwa kama usemaji tofauti baina ya wazungumzaji wa lugha moja ambao unaweza kusababishwa na utofauti wa utengano wa muda mrefu, kijiografia, sababu za kiuchumi, kijamii ama kisiasa ambazo husababisha baadhi ya watu wa jamii moja kuhama na kwenda sehemu ya mbali katika kutafuta amani ama riziki. Wakati lahaja inahusika na eneo dogo kijiografia, lugha huweza kutumika katika eneo kubwa kijiografia. Kwa mfano, lugha ya Kiswahili inatumika na jamii mbalimbali za watu wa ndani na nje ya Afrika Mashariki tofauti na lahaja[3] kama vile Kimakunduchi ambayo hutumiwa na watu waliopo Kusini Unguja[4] na Kipemba ambayo hutumiwa na jamii ya watu wa kisiwa cha Pemba[5].

## 2.0 Fasili na Chanzo cha Mbinu Linganishi

Fox (1995: 4) anaeleza kuwa Mbinu Linganishi ni mbinu inayotumika katika ulinganishi wa lugha mbalimbali nayo ni ya msingi sana na ya mwanzoni miongoni mwa mbinu za uundaji upya kwa sababu utambuzi wa historia ya lugha mbalimbali umetokana na matumizi ya mbinu hii. Anaendelea kufafanua zaidi kuwa, Mbinu Linganishi inahusishwa na taaluma ya historia[6] ya lugha kutokana na kujihusisha kwake na ulinganishi wa kifilolojia na ulinganishi wa kiisimu.

Kwa mujibu wa Rankin (2007: 1) Mbinu Linganishi ni seti ya mbinu/njia zilizoanzishwa zaidi ya karne moja na nusu, nazo husaidia kuunda isimu ya mwanzo ambayo ni thibitifu katika lugha husianifu za Mame lugha-moja. Rankin anafafanua kwamba, vipengele vya uundaji vya Mame lugha-moja vinaweza kuwa fonolojia, mofolojia, sintaksia, msamiati, semantiki n.k. Pia, vipengele vya uundaji vinaweza kuwa faridi za vipengele hivyo (yaani fonimu, mofimu, maneno n.k.) au hata kanuni, mashartizuizi na mazingira kutegemea modeli ya sarufi inayotumiwa. Rankin anasema kuwa Mbinu Linganishi zinahusisha ulinganishi wa vipengele mnasaba kutoka katika lugha mbili au zaidi zinazohusiana. Mara nyingi ulinganishi unaotumia mbinu hii huhusisha maneno mnasaba ya msamiati wa msingi na upembuzi wa sauti mrejeo na mwisho uundaji wa mfumo mame wa kifonolojia na msamiati.

Wataalamu wengine walioelezea maana ya Mbinu Linganishi ni James na Malande (2012) ambao wanasema kuwa, ni utaratibu wa ulinganishi wa lugha unaolenga kubaini uhusiano baina yake, kubainisha lugha zilizotokana na Mame lugha fulani, na kuukilia uhusiano wa karibu baina ya lugha zinazolinganishwa. Kwa upande wake Massamba (2016: 72) anaeleza kuwa, Mbinu Linganishi ni

---

[3] Lahaja ndizo zilizozaa Kiswahili kinachozungumzwa na jamii kubwa ukilinganisha na jamii zinazozungumza lahaja. Kwa ufafanuzi zaidi tazama Mbaabu (2007).

[4] Tazama Iddi (2011) na Hans (2014) kwa maelezo zaidi kuhusu mahali inakozungumzwa lahaja ya Kimakunduchi

[5] Tazama Juma (2011) na Hans (2014).

[6] Elimu maalumu inayohusiana na matukio na mambo yaliyopita (TUKI, 2013).

mbinu ya kiuchunguzi na kiuchambuzi itumiayo taratibu mbalimbali kuunda upya historia ya lugha mbili au zaidi zisemekanazo kuwa na asili moja.

Kwa ujumla, Mbinu Linganishi ni mbinu ya kiuchunguzi na kiuchambuzi iliyoibuka baada ya wanazuoni mbalimbali kama vile Bopp (1816), Grimm (1822), Schleicher (1850, 1861 & 1873) na Verner (1875) kama wanavyoelezwa katika Fox (1995) kujikuta wakilinganisha lugha mbalimbali ulimwenguni pasi kutumia utaratibu maalumu na wa kisayansi. Hivyo, wakajikuta wanakwama katika baadhi ya mambo wakati wa ulinganishi. Chanzo cha mbinu hii ni isimu linganishi na isimu historia. Mwaro (2003) anaeleza kuwa isimu linganishi ilianza karne ya 16 ilhali wanaisimu wengine kama vile Fox (1995), Hock na Joseph (1996) wanasema kuwa ilianza karne ya 15. Uanzishwaji wa isimu linganishi ulitokana na mahitaji ya wanafilolojia[7] kulinganisha vipengele mbalimbali vya lahaja na lugha ambavyo vilionekana kuhitaji kulinganishwa. Isimu historia inadaiwa kuanzishwa katika karne ya 18 nayo inasemekana ilitokana na fikra za Aristotle na Plato walioonekana kuitazama lugha kwa msingi wa kimantiki na kilumbi (Mwaro, 2003). Massamba (2009: 20) anasema kuwa, isimu historia ni taaluma ya isimu ambayo hutalii mabadiliko mbalimbali ya lugha kadiri miaka inavyopita. Kwa upande wa Obuchi na Mukhwana (2015) isimu historia ni tawi linaloshughulikia maendeleo na mabadiliko ya lugha kiwakati kutoka kipindi kimoja cha historia hadi kingine, ikiwa ni pamoja na sababu na matokeo ya mabadiliko hayo.

Obuchi na Mukhwana wanaeleza zaidi kwamba isimu historia hufafanua mabadiliko yanayotokea katika lugha mahususi kando na kutoa maelezo kuhusu historia ya lugha mbalimbali ili kuonyesha namna lugha hizo ama zinavyotofautiana au zinavyoelekea kufanana. Isimu historia hudhihirisha mabadiliko ya sauti, maumbo ya maneno, sentensi na maana za maneno, kihistoria. Mbali na mambo mengine isimu historia huchunguza mabadiliko ya lugha katika mapito ya nyakati na huangaza jinsi lugha inavyobadilika katika vipindi mbalimbali, sababu za mabadiliko hayo na athari zake katika lugha hiyo. Kwa ujumla, isimu historia hujishughulisha na mabadiliko yanayotokea katika lugha kwa kumakinikia katika vipengele mbalimbali vya lugha ikiwemo historia yake kwa lengo la kufahamu mnasaba wake. Uchunguzi wa mabadiliko yanayotokea katika lugha umekuwa ukifanyika kwa kutumia Mbinu Linganishi.

Kumekuwa na mitazamo mbalimbali kuhusu mwasisi wa Mbinu Linganishi. Baadhi ya wanazuoni kama vile Fox (1995: 17-19), Joseph na Hock (1996: 35-41, 455) na Beeks (2011) wanasema kwamba mwasisi wake ni William Jones mnamo mwaka 1786. Madai haya yanatofautiana na wanazuoni kama vile Luraghi na Bubenik (2010: 7-8) ambao wanasema kuwa kabla ya William Jones, kuna mwanazuoni anayejulikana kwa jina la Jesuit Janos Sajnovics aliyetumia Mbinu Linganishi katika kuhusianisha mofimu ambatani za lugha za Kilapu na Kihungaria. Fox (1995: 4) anaeleza kuwa, hapo awali suala la ulinganishi

[7] Ni neno linalotokana na filolojia, taaluma inayojishughulisha na asili na maendeleo ya lugha au lahaja.

lilikuwapo isipokuwa halikuwa likifanywa kwa kuzingatia utaratibu maalumu. Sababu ya kutozingatia utaratibu huo zinatajwa kuwa wanazuoni hao wa awali mathalani wale wa karne ya 18, walijikita katika uegemeo wa kifalsafa zaidi kuliko uegemeo wa kiisimu. Pia, wanazuoni walio wengi hawakujua kuwa utambuzi wa uhusiano wa kihistoria baina ya lugha unahitaji ulinganishi wa lugha husika. Kuanzia karne ya 19 ndipo wanaisimu mbalimbali walipoanza kuchunguza uhusiano baina ya lugha kwa kuzilinganisha kiutaratibu. Hivyo, katika karne hiyo ulinganishi ukawa wa kiutaratibu, kuaminika na wa kisayansi zaidi. Miongoni mwa wataalamu walioitumia Mbinu Linganishi katika kubaini uhusiano baina ya lugha mbalimbali kwa Ulaya ni Bopp (1816), Grimm (1822), Schleicher (1850, 1861 & 1875), Meillet (1925 & 1937), Anttila (1972), Fox (1995), Hock na Joseph (1996), Beeks (2011) kwa kuwataja wachache.

## 3.0 Dhima za Mbinu Linganishi

Mtafiti katika makala hii amegawa dhima za Mbinu Linganishi katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni la kihistoria, la pili ni la kiisimu na la tatu ni la kijamii kama inavyojadiliwa katika sehemu ifuatayo:

### 3.1 Kubainisha Asili na Chimbuko la Lugha/Lahaja

Dhima za Mbinu Linganishi zinasaidia kujua chimbuko halisi la lugha mbalimbali za ulimwenguni kwa kulinganisha historia za makundi ya lugha yanayohusika. Hivyo, Mbinu Linganishi inasaidia wanaisimu kubainisha chimbuko asilia la makundi ya lugha yanayolinganishwa. Kwa mfano, kutokana na matumizi ya Mbinu Linganishi katika ulinganishi wa lugha mbalimbali za Kibantu uliofanywa na wataalamu mbalimbali kama vile Johnston (1919), Greenberg (1955) pamoja na Guthrie (1970), imesababisha kuwapo kwa mitazamo tofauti juu ya chimbuko la lugha hizo. Mitazamo hiyo imetokana na baadhi ya wanaisimu kutokuitumia kiufasaha mbinu linganishi. Mathalani, baadhi ya wanazuoni kama vile Greenberg (1955) katika utafiti wake anadai kuwa chimbuko la lugha za Kibantu ni maeneo ya Kameruni-Nigeria. Naye Guthrie (1948, 1967, 1970 & 1971) katika uchunguzi wake wa lugha 200 alibaini kuwa chimbuko la lugha za Kibantu ni Zambia, huku Nurse na Spear (1985) na Massamba (2002 & 2007) wanaona kuwa chimbuko la lugha za Kibantu ni Pwani ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, si lengo la makala hii kujishughulisha na chimbuko sahihi la wazungumzaji wa lugha za Kibantu, bali madhumuni ya makala hii ni kujadili dhima za Mbinu Linganishi katika uhusiano baina ya lugha na lahaja.

Vilevile, katika dhima hii ya kihistoria Mbinu Linganishi zinasaidia kubaini mabadiliko yanayozikumba lugha mbalimbali ulimwenguni kulingana na wakati. Lugha yoyote hai, kwa maana ya lugha zenye wazungumzaji, zipo katika mabadiliko. Mabadiliko ya lugha yoyote ile huenda sambamba na mabadiliko ya kijamii katika nyanja zake mbalimbali kisiasa, kiutamaduni, kijamii, kisayansi na kiteknolojia. Mabadiliko yanayoikumba jamii yanahusisha uibukaji wa dhana

mbalimbali ambazo huchangia katika mabadiliko ya lugha. Mbali na mambo mengine, maendeleo mbalimbali yanayotokea katika jamii husababisha jamii kuingiliana kwa kiasi kikubwa. Matokeo ya mwingiliano huo husababisha mabadiliko katika lugha, ambayo huhusisha vipengele mbalimbali vya lugha kama vile fonolojia, mofolojia, sintaksia na msamiati. Kwa mfano, maneno yafuatayo yanaonesha mabadiliko ya kimsamiati katika lugha ya Kimakonde:

**Jedwali la 1: Mabadiliko ya Kimsamiati katika lugha ya Kimakonde**

| **Kabla ya mabadiliko** | **Baada ya mabadiliko** | **Kabla ya mabadiliko** | **Baada ya mabadiliko** |
|---|---|---|---|
| *kunyata* | baya | *twala* | beba |
| *chikulu* | kubwa | *lombwa* | olewa |
| *livelya* | linyoya | *veleka* | zaa |

**Chanzo**: Mtafiti (2016)

Mifano hii inaonesha mabadiliko ya kimsamiati yaliyotokana na mwingiliano baina ya Kimakonde na Kiswahili. Mabadiliko hayo ya kimsamiati ni matokeo ya 'nipe nikupe' msamiati baina ya wazungumzaji wa Kiswahili na Kimakonde. Kuwapo kwa mabadiliko hayo kumesababisha uibukaji wa visawe mbalimbali katika lugha ya Kimakonde, kwa mfano, kisawe cha neno *kunyata*[8] ni 'baya', na kisawe cha neno *chikulu* ni 'kubwa'.

## 3.2 Kubainisha Vipengele vya Kiisimu vya Lugha Mbalimbali

Mbinu Linganishi ina dhima mbalimbali za kiisimu. Kwanza kabisa inasaidia kubainisha vipengele tofauti vya kiisimu ambavyo kundi fulani la lugha linavyo au linakinzana. Kwa mfano, makundi mbalimbali ya lugha kimuundo ni matokeo ya Mbinu Linganishi ambapo wanaisimu walikaa na kuchunguza vipengele anuwai vya kimofolojia na kubainisha makundi tofautitofauti ya lugha kulingana na sifa changiani[9]. Mathalani, lugha tenganishi, lugha ambishi, lugha ambishi bainishi, lugha ambishi mchanganyo na lugha muundo gubi (Mgullu, 2010) ni mifano ya makundi ya lugha kimuundo yaliyogawanywa kutokana na mbinu linganishi. Pili, Mbinu Linganishi husaidia kuelewa sifa majumui za lugha ulimwenguni. Inaposemwa kwamba lugha zote zina irabu na konsonanti au lugha zote zina silabi, hoja hii haikuibuka kiholela bali ni kwa mujibu wa jopo la wanazuoni waliofanya uchunguzi kwa kutumia Mbinu Linganishi. Tatu, Mbinu Linganishi inasaidia kubainisha sifa bainifu za kundi fulani la lugha. Kwa mfano, inaposemwa kuwa kundi la lugha fulani lina toni ama lina mkazo ni madai ambayo ni matokeo ya ulinganishi wa kundi fulani na kundi jingine. Nne, Mbinu Linganishi inasaidia

---

[8] Neno hili halitumiki tu katika lugha ya Kimakonde bali linatumika pia katika lugha nyingine za mikoa ya kusini mwa Tanzania kama vile Kimatumbi, Kimwera na Kimakua.

[9] Sifa zilizoonekana kufanana kati ya kundi moja la lugha na jingine.

kubainisha sifa ambazo ni za kipekee katika kundi au makundi fulani ya lugha. Mathalani, baadhi ya lugha kama vile Kifaransa hazina sauti /r/[10] hususan wakati wa utamkaji sauti hizo huwa katika tahajia tu na sio matamshi. Kwa mfano maneno *père* (baba) inatamkwa [pɛR] na *mère* (mama) inatamkwa [mɛR] lakini mzungumzaji wa Kiswahili anaweza kutamka [pɛrɛ] na [mɛrɛ] mtawalia kwa kuwa katika Kiswahili hakuna sauti [R]. Kiingereza na Kiswahili zinatumia sauti [r], kwa mfano, katika maneno kama ‘roho’ na ‘rasimu’.

### 3.3 Kubainisha Uhusiano baina ya Jamiilugha Mbalimbali

Kama ilivyo ada ya lugha kutowezekana kutenganishwa na jamii, ndivyo ilivyo pia kuzungumzia dhima za Mbinu Linganishi pasi kugusia suala la jamii. Lugha na jamii ni mambo ambayo ni vigumu kuyatenganisha kwa sababu lugha hutumiwa na binadamu ambaye ni sehemu ya jamii fulani. Kwa mfano, tunaposema kwamba ‘yule ni Mmakonde’, hii ina maana kuwa mtu husika anazungumza Kimakonde lakini pia asili yake ni jamii ya Kimakonde. Ni vigumu kusema ‘yule ni Mchina’ ilhali anatokea katika jamii yenye kuzungumza lugha ya Kiswahili na wazazi wote wa pande mbili ni Waswahili.

Mbinu Linganishi kijamii inasaidia kubainisha uhusiano baina ya jamiilugha mbalimbali. Hii ina maana kuwa kuna wakati wanajamii wanaweza wasijue kama wana uhusiano na jamii fulani lakini baada ya kufanyika ulinganishi wanaweza wakafahamu kwamba wanahusiana kwa namna fulani na jamiilugha hiyo. Kwa mantiki hiyo, Mbinu Linganishi husaidia kuleta uelewano baina ya jamii moja na nyingine, hasa baada ya jamii hizo kutambua kuwa kuna uhusiano wa namna fulani katika lugha zao. Mathalani, utafiti wetu unaonesha kuwa baadhi ya watu kutoka Makunduchi na maeneo mengine ya visiwa vya Zanzibar asili yao ni kutoka Tanzania Bara. Wanajamii hao walijikuta wakichangamana na kuingiliana kutokana na sababu mbalimbali za kijamii kama vile ndoa, dini, biashara, utamaduni na nyinginezo. Mfano ufuatao kutoka kwa mtoa taarifa wa Paje, Makunduchi unafafanua zaidi;

> Sasa unajua halafu kuna watu ambao wametoka sehemu mbalimbali mfano kama kutoka huko bara kama watumwa eeeh watu kutoka sehemu za Kongo, Songea, Sumbawanga, Iringa na Bagamoyo. Watu wenye asili tofautitofauti walikuja hapa lakini wakawa watu wa Paje[11].
>
> **Chanzo**: Mtafiti (2016).

Katika maelezo haya tunaona namna watu wa Makunduchi walivyoingiliana na watu wa maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara na kwingineko.

Mbali na mambo mengine, mfungamano baina ya lugha za Kibantu na lahaja huwasaidia wanaisimu kutambua namna kundi au makundi fulani ya lugha yanavyohusiana. Hii ina maana kwamba lugha zilizopo katika kundi moja huwa na

---

[10] Kwa ufafanuzi zaidi juu ya tofauti za sauti [r] na [R] tazama Katamba (1996: 13) na Omary (2002).

[11] Ni miongoni mwa Shehia zilizopo katika wilaya ya Makunduchi katika mkoa wa Kusini Unguja mahali kulikofanyika utafiti huu.

vipengele mbalimbali ambavyo hufanana na/au kutofautiana. Uhusiano huo wa lugha unaweza kutokana na vipengele vya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, kisemantiki au kihistoria. Mathalani, mfanano wa kihistoria unasababishwa na kundi fulani la lugha kuchangia asili au chimbuko. Kwa mfano, lugha nyingi za Kibantu chimbuko lake ni Afrika Mashariki (taz. Nurse na Spear, 1985; Massamba, 2002 & 2007). Kuna mambo mbalimbali yanayoweza kuhusishwa na uhusiano baina ya lugha na lugha ama lugha na lahaja. Aidha, ni vigumu kueleza uhusiano baina ya lugha na lugha au lugha na lahaja bila kutumia Mbinu Linganishi. Kuibuka kwa Mbinu Linganishi kulitokana na hamu ya wanaisimu kubainisha uhusiano baina ya lugha. Hivyo basi, ni ukweli usiopingika kuwa mbinu hii huenda sambamba na suala la uhusiano baina ya lugha. Kwa ujumla, Mbinu Linganishi haiwezi kuzungumziwa pasi kuelezea uhusiano baina ya lugha; kipengele § 3.3.1 kinajadili suala hili na kipengele § 3.3.2 mjadala unahusu uhusiano baina ya lahaja na lugha za Kibantu.

### 3.3.1 Uhusiano baina ya Lugha

Uhusiano baina ya lugha ni hali ya kuwapo kwa sifa fulani baina ya lugha au kundi fulani la lugha na jingine zinazofanana au kuelekeana (Massamba, 2016). Suala la uhusiano baina ya lugha si kitu kigeni katika uga wa isimu kwa sababu tangu karne nyingi zilizopita wanaisimu wamekuwa wakijishughulisha nalo. Kitu kilichowavutia zaidi wanaisimu hao ni kutaka kujua zaidi mambo yanayosababisha lugha fulani ziwe na mfanano au uhusiano. Uhusiano baina ya lugha ulianzia Ulaya ambapo wanaisimu mbalimbali Kabla ya Kristo na Baada ya Kristo walitamani kujua chimbuko hasa la lugha zao na lugha nyinginezo ili kufahamu kama ni za mnasaba mmoja au la. Kwa upande wa lugha za Kiafrika, mathalani lugha za Kibantu, wanaisimu mbalimbali walijihusisha na kuangalia uhusiano baina ya lugha hizo. Baadhi ya wanaisimu hao ni Johnston (1919), Greenberg (1955), Guthrie (1948, 1967, 1970 & 1971), Nurse na Spear (1985), Maho (1999), Hombert na Hyman (1999), Masele (2001), Massamba (2002) na Dimendal (2011). Pamoja na wataalamu tajwa kuangalia uhusiano wa lugha za Kibantu, Mekacha (2011) anaelezea ugumu wa kubainisha uhusiano wa lugha za Tanzania. Ugumu huo unatokana na sababu za kihistoria, kwamba ni vigumu kutofautisha lugha na kabila. Aidha, makisio ya lugha za Tanzania yanaonesha kuwa kila jamii ni kabila moja na kila kabila lina lugha moja. Hata hivyo, kuna mbari[12] za lugha mbalimbali zinazotajwa kuwapo katika Bara la Afrika. Mbari hizo ni pamoja na;

a) Lugha za Kikhoisani kama vile Kisandawe na Kihadza zinazozungumzwa katika maeneo ya kaskazini kidogo ya katikati mwa Tanzania hususan mikoa ya Dodoma na Arusha. Wazungumzaji wa Kikhoisani wanasemekana kuwa ndiyo wa kwanza kukalia maeneo ambayo hivi sasa ni Tanzania tangu yapata miaka 5000 hivi iliyopita..

[12] watu wa kitovu kimoja; jamii, kabila ukoo (TUKI, 2004:229).

b) Lugha za Kikushiti ni lugha za tawi mojawapo la mbari ya Afroasia. Lugha hizi ambazo zinazungumzwa katika maeneo ya katikati mwa Tanzania ni pamoja na Kiiraqwi, Kiburunge, Kialangwa, Kiisaax, Kigorowa na Kima'a. Wazungumzaji wake wengi wapo Dodoma na Arusha. Inasemekana kwamba wazungumzaji hao walitokea Somalia na Ethiopia na kuhamia maeneo ambayo hivi sasa ni Tanzania yapata miaka kama 2000 hivi iliyopita.

c) Lugha za Kiniloti ni lugha za mbari ya Nilo-Sahara. Mifano ya lugha hizo ni pamoja na Kidatoga na Kiakie, Kimaasai, Kiongamo na Kiluo nchini Tanzania. Lugha za Kibantu ni kundi kubwa la lugha nchini Tanzania nalo ni tawi mojawapo la mbari ya Niger-Kongo.

Pamoja na ugumu huo uliobainishwa na Mekacha wanaisimu-linganishi hawajakoma kulinganisha lugha mbalimbali za Kibantu na kuibuka na matokeo ya namna mbalimbali.

### 3.3.2 Uhusiano baina ya Lahaja na Lugha za Kibantu

Wanazuoni mbalimbali wameeleza na kutaja uhusiano baina ya lugha za kijamii na lahaja (taz. Mkude, 1983; Nurse na Spear, 1985; Chum, 1994; Massamba, 2002 & 2007; Hans, 2014). Kwa mfano, Mkude (1983) anaeleza kuwa karibu kila lahaja ya Kiswahili inaelekea kubebana na lugha ya Kibantu. Anasisitiza kwamba wazungumzaji wa lahaja za Kiswahili hawawezi kutengwa na Wabantu wengine mgongoni mwao. Mbali na Mkude, Abdul Wakil mwaka 1993 katika dibaji ya Chum (1994: 4) anaeleza kuwa kuna uhusiano baina ya lahaja ya Kimakunduchi na lugha nyinginezo za Tanzania Bara, Kenya na kwingineko hasa pale anaposema kuwa:

> Kikae ni Kiswahili ambacho husemwa huko Makunduchi, yaani Kae. Lakini ndani yake yamo maneno mengi sana ambayo hayana asili ya Kiswahili. Inawezekana maneno hayo yameazimwa kutoka katika lugha kadha zisemwazo Tanzania Bara, Kenya na kwingineko. Vilevile, ni shida sana kwa mtu ambaye hakuzaliwa na hasa kukulia Makunduchi kuweza kukisema kwa fasaha nzuri. Watu wengi hujaribu kukisema lakini mara hushindwa katika matamshi. Kwa sababu hiyo baadhi ya watu hufikiri Kikae ni lugha tofauti na Kiswahili.
>
> **Chanzo**: Chum (1994: 4)

Katika maelezo haya inaoneshwa wazi kuwa kuna uhusiano baina ya lahaja na lugha nyingine za Kibantu za Tanzania Bara, Kenya na kwingineko. Vilevile, Juma (2011) anaeleza kuwa kuna uhusiano wa kiutamaduni baina ya wazungumzaji wa lugha za Kibantu (tofauti na Kiswahili) za Tanzania Bara na lahaja za Kiswahili za Zanzibar. Maelezo yafuatayo yanafafanua zaidi:

> Watu wanaoishi Wete ni mchanganyiko kutoka vijiji mbalimbali vya Pemba, nje ya Pemba na wenye asili ya Asia. Watu wa Wete wana utamaduni mchanganyiko kwani upo utamaduni unaopatikana sehemu za bara, na pia kuna utamaduni wa kigeni, kama vile wa Kiarabu na Kiajemi. Chanzo: Juma (2011:4)

Katika maelezo hayo inaonekana kuwa kuna uhusiano wa kiutamaduni baina ya watu wa Pemba na wale wanaotokea katika maeneo mengine kama Tanzania na Kenya. Kwa kuwa lugha ni kipengele kimojawapo cha utamaduni na ni nyenzo mojawapo inayotumika kuuelezea utamaduni wa mahali fulani, tunathubutu kusema kuwa uhusiano huo hauishii tu katika utamaduni bali pia hata katika lugha.

Pamoja na wanazuoni mbalimbali kuzungumzia suala la lugha za Kibantu na lahaja zake, wengi wao wameeleza juu juu bila kuwa na data za kutosha pengine kwa sababu hayakuwa malengo ya kazi zao. Kwa mfano, Mwashota (2012) na Mwanyanje (2012) wametaja kuwa katika lugha ya Kisafwa inayopatikana katika mkoa wa Mbeya kuna lahaja tano. Lugha hiyo ya Kisafwa imeelezwa na Mwashota (2012) kuwa inazungumzwa katika maeneo mbalimbali ambayo ni wilaya ya Mbeya Vijijini, Chunya, Rungwe, Mbeya Mjini na kwa kiasi kidogo katika wilaya ya Mbozi. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya mgawanyo wa mikoa tunaweza kusema kuwa Kisafwa kinazungumzwa katika mkoa wa Mbeya na mkoa wa Songwe. Katika mkoa wa Mbeya, Kisafwa kinazungumzwa katika wilaya tatu yaani, Mbeya Vijijini, Rungwe na Mbeya Mjini. Kwa upande wa mkoa wa Songwe, lugha hii inazungumzwa katika wilaya ya Momba na Chunya. Aidha, suala la Mwashota na Mwanyanje kutaja kwamba Kisafwa kina lahaja tano bila kufanya uchunguzi wa kina ni tatizo kubwa. Kwa mantiki hiyo, utafiti wa kina utakaotumia Mbinu Linganishi kiufasaha unahitajika ili kuibuka na data jarabati zitakazothibitisha kuwapo kwa lahaja hizo. Pia, tukiangalia katika lugha ya Kimakonde kuna baadhi ya wanaisimu kama vile Kraal (2005) wanaeleza kwamba katika lugha hii kuna lahaja mbalimbali kama vile Kinnima, Kindonde, Kimatambwe na Kimalaba pasi kufanya ulinganishi wa kina kwa kutumia Mbinu Linganishi. Hivyo basi, kuna haja ya kufanya utafiti wa kiisimu-historia linganishi utakaotumia mipaka ya Mbinu Linganishi ipasavyo ili kulinganisha hizo zinazotajwa kuwa ni lahaja za baadhi ya lugha za Kibantu.

## 4.0 Mipaka ya Mbinu Linganishi

Mbinu Linganishi ina mipaka yake. Baadhi ya mipaka hiyo ni:

a) Mipaka ya muda wa uhusiano: humaanisha kwamba kadiri mabadiliko yanavyozidi kutokea katika lugha ndivyo mbinu hii inavyopunguza makali yake ya kubainisha uhusiano;
b) Mipaka ya historiajamii: ni hali fulani ya kihistoria inayosababisha athari za kiisimu katika mbinu linganishi;
c) Mipaka ya kiisimu: inamaanisha kwamba, ni baadhi tu ya vipengele vya kiisimu ndivyo vinaweza kulinganishwa kisawasawa;
d) Mipaka ya upekee: inazingatia uhusiano wa uasilia (kijenetiki tu) ili kufikia hitimisho la aina ya uhusiano.

Mipaka iliyobainishwa hapo juu inaonesha kwamba Mbinu Linganishi haitumiki kiholela bali ina kaida zake zinazoenda sambamba na mipaka. Kaida hizo hazina budi kuzingatiwa katika ubainishaji wa uhusiano baina ya lugha au baina ya lugha

na lahaja. Kwa mfano, mpaka (b) unazungumzia historiajamii kwamba jamii yoyote ile ina historia yake ambayo ni matokeo ya mambo mbalimbali yanayoihusu. Historiajamii huwawezesha wanaisimu-linganishi kubaini asili ya lugha zinazolinganishwa kama zina mnasaba mmoja au la.

## 5.0 Hitimisho

Kwa ujumla, makala hii imejadili dhima za Mbinu Linganishi katika kuhusisha lugha na lahaja. Katika kujadili dhima hizo imebainika kwamba Mbinu Linganishi husaidia kubainisha chimbuko na asili ya lugha/lahaja mbalimbali na vipengele tofautitofauti vya kiisimu vya lugha zilizolinganishwa. Vilevile, mbinu hii imesaidia kubaini uhusiano baina ya jamiilugha. Aidha, mtafiti amegundua kwamba kuna tatizo katika tafiti zilizofanywa na wanazuoni mbalimbali kuhusu uhusiano baina ya lugha na lugha, pia uhusiano baina ya lugha na lahaja. Tatizo hili limetokana na baadhi ya wanaisimu kutoa maelezo ya jumla kuhusu uhusiano uliopo baina ya lugha na lahaja suala linalosababisha mkanganyiko. Mkanganyiko huo unatokana na kukosekana kwa matumizi bora ya Mbinu Linganishi na/au kutozingatia mipaka ya mbinu linganishi. Hivyo basi, kuna haja ya kutumia Mbinu Linganishi vizuri ili kubainisha uhusiano baina ya lugha na lugha ama lugha na lahaja. Zaidi ya hayo, utafiti wa uhusiano baina ya lugha na lugha na lugha na lahaja unapaswa kuwa endelevu kwa sababu lugha si tuli bali inabadilika kila leo; kubadilika kwa lugha ndiyo maendeleo yenyewe ya lugha. Maendeleo hayo yanaweza kuwa ni ya kimsamiati, kifonolojia, kimofolojia na kisemantiki.

## Marejeleo


Amani. H. (2010). The Influence of Kiswahili in Kimalaba: A Case of Lexical and Structure Borrowing. Unpublished MA Dissertation, University of Dar es Salaam.

Anttila, R. (1972). An Introduction to Historical and Comparative Linguistics. New York: Macmillan Publishing Co. Inc

Beeks, R. S. P. (2011). *Comparative Indo-European Linguistics*. Philadelphia: John Benjamin Publishing Company.

Bopp, F. (1816). *Über das Konjugationssystem der Sanskritspraches in Vergleichung mit Jehem der Griechischen, Lateinischen, Persischen und Germanischen Sprache*. Frankfurt.

Chum, H. (1994). *Msamiati wa Pekee wa Kikae*. Uppsala: Nordic Association of African Studies.

Dimmendal, G. J. (2011). *Historical Linguistics and the Comparative Study of African Languages*. University of Cologne: John Benjamins Publishing Company.

Fox, A. (1995). *Linguistic Reconstruction: An Introduction to Theory and Method*. New York: Oxford University Press.

Greenberg, J. (1955). *Studies in African Linguistics Classification.* Connecticut: New Haven.
Grimm, J. (1822). *Deutsche Gramatik*. Göttingen: Dietrich.
Guthrie, M. (1948). *The Classification of Bantu Languages*. London: OUP.
Guthrie, M. (1967). *Comparative Bantu*. Vol. 1 Farnborough: Gregg International Publishers.
_______(1970). *Comperative Bantu*. Vol. 2 Farnborough: Gregg International Publishers.
_______(1971). *Comparative Bantu*. Vol. 4 Farnborough: Gregg International Publishers.
Hans, M. M. (2014). Mchango wa Lahaja katika Kukuza na Kuendeleza Kiswahili Sanifu: Hazina Fiche iliyomo katika Lahaja za Kiswahili za Zanzibar. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
Hock, H. H. na Joseph, B. D. (1996). *Language History, Language Change and Language Relationship: An Introduction to Historical and Comparative Linguistics*. New York: Mouton de Gruyter.
Hombert, J. M. na Hyman, L. M. (Wah.) (1999). *Bantu Historical Lingustics: Theoretical and Empirical Perspectives*. California: CSLI Publication.
Iddi, Z. A. (2011). Phonological Processes in Kimakunduchi. Unpublished MA Dissertation, University of Dar es Salaam.
James, M. na Malande, O. (2012). *An Introduction to Language and Linguistic Theory: With Insights from African Languages*. Mwanza: Serengeti Bookshop.
Johnston, H. (1919). *A Comparative Study of the Bantu and Semi-Bantu Languages*. Oxford: Clarendon Press.
Juma, H. K. (2011). Tofauti za Kiisimu baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili cha Wete katika Kisiwa cha Pemba. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
Katamba, F. (1996). *An Introduction to Phonology*. London and New York: Longman.
King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimujamii.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
Kraal, P. J. (2005). A Grammar of Kimakonde. Unpublished PhD Thesis. Leiden University. Department of African Studies.
Luraghi, S na Bubenik, V. (2010). *Continuum Companion to Historical Linguistics*. New York: Continuum International Publishing Group.
Maho, J. F. (1999). *A Comparative Study of Bantu Noun Classes*. Göteborg: Göteborg University.
Masele, B. F. Y. P. (2001). The Linguistic History of Sisuumbwa, Kisukuma and Kinyamwezi in Bantu Zone F. Unpublished PhD. Thesis, Memorial University of Newfoundland.

Massamba, D. P. B. (2002). *Historia ya Kiswahili: 50BK hadi 1500BK.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

______(2007). *Kiswahili Origins and the Bantu Divergence- Convergence Theory*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

______(2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha* (Toleo la pili). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

______(2016). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha* (Toleo la tatu). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Meillet, A. (1925). *La Méthode Comparative en Linguistique Historique*. Oslo: Aschehaug.

Meillet, A. (1937). *Introduction à l'étude Comparative des Langues Indo Européennes*. Paris: Champion.

Mekacha, R. D. K. (2011). *Isimujamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Mgullu, R. S. (2010). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mkude, D. (1983). "Mtawanyiko wa Lahaja za Kiswahili" katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili, Lugha ya Kiswahili*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. 1: 65-88.

MLUTA (2009). *Atlasi ya Lugha za Tanzania*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mwanyanje, W.T. (2012). Shisafwa Noun Phrase Structure. Unpublished MA Dissertation, University of Dar es Salaam.

Mwaro, G. W. (2003). "Dhana ya Kubadilika kwa Lugha katika Isimu-Historia-
Linganishi: Mifano Kutoka Kiswahili. Katika *Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. 66: 25-38.

Mwashota, P. (2012). Ruwaza za Uradidi wa Vitenzi katika Lugha ya Shisafwa. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nurse, D. na Spear, T. (1985). *The Swahili: Reconstructing the History and Language of An African Society*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Obuchi, S. M. na Mukhwana, A. (2015). *Muundo wa Kiswahili Ngazi na Vipengele*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Omary, S. (2002). Pronunciation Problems that Tanzanian Learners Encounter in Learning French. Unpublished MA Dissertation, University of Dar es Salaam.

Rankin, R. L. (2007). "The Comparative Method: The Handbook of Historical Linguistics", Blackwell Reference Online.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Tatu). Nairobi: Oxford University Press.

Schleicher, A. (1850). *Linguisticsche*. Bonn: Untersucchugen.
Schleicher, A. (1861). *Compendium der Vergleichenden Grammatik der Indogermanischen Sprachen*. Weimar: Böhlau.
Schleicher, A. (1873). *Die Darwinsche Theorie und die Sprachwissen Schaft*. Toleo la pili. Weimar: Böhlau.
Verner, K. (1875). "Eine Ausnahme der Ersters Lautverschiebung". Katika *Zeit-Schrift für Vergleichende Sprachforschung.* 23: 97-130.